

# HABARILEO

GAZETI DADA LA DAILY NEWS ISSN 1821-570X TOLEO NA 01398 JUMANNE OKTOBA 19, 2010 TSH. 400 KSH. 40

TANZANIA

## Wagonjwa 23 wapelekwa India kwa matibabu

Na Mwandishi Wetu

**W**AGONJWA wa moyo 23 wengi wao wakiwa ni watoto wameondoka nchini kwenda India kwa ajili ya upasuaji wa moyo.

Watoto hao wakiwa na wasindikizaji wao waliondoka juzi na jana katika uwanja wa kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere Dar es Salaam na waliagwa na viongozi wa Lions Klabu ya Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa hospitali ya Regency inayoratuibu safari hiyo, Dk. Rajni Kanabar watoto hao watatibiwa katika hospitali ya Fortis Escorts iliyoko katika mji wa New Delhi India.

Alisema wanatarajiwa kuwasili nchini baada ya wiki nne za matibabu na aliwashukuru wasamaria mbalimbali ambao walijitokeza kutoa michango ya hali na mali kufanikisha safari hiyo ili kuokoa maisha ya watoto hao akiwemo mfanyabiashara maarufu, Jafu Sabodo ambaye alitoa dola za Marekani 20,000 kwa ajili ya wagonjwa hao.